



BODI YA BIMA YA AMANA

KATIKA SHAURI LA FBME BANK LTD (CHINI YA UFILISI) NA

KATIKA SHAURI LA SHERIA YA MABENKI NA TAASISI ZA FEDHA, 2006 (THE BANKING AND FINANCIAL INSTITUTIONS ACT, 2006)

TAARIFA KWA UMMA

TAARIFA inatolewa kwa umma kwamba **FBME BANK LTD** imewekwa chini ya ufilisi na Benki Kuu ya Tanzania kuanzia tarehe 8 Mei, 2017. Kwa mamlaka iliyopewa chini ya kifungu cha 61 (1) na 41 (a) cha Sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha, 2006 (The Banking and Financial Institutions Act, 2006) Benki Kuu ya Tanzania imeiteua Bodi ya Bima ya Amana (Deposit Insurance Board –DIB) taasisi iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 37 (1) cha Sheria tajwa kuwa Mfilisi wa Benki hiyo.

Kufuatia uteuzi huo, Mfilisi wa **FBME BANK LTD**, Bodi ya Bima ya Amana (DIB), inatoa taarifa kwa wadai na wadaiwa wote wa benki hiyo kama ifuatavyo;

- (a) Wadaiwa wote wa **FBME Bank Ltd** na mtu yoyote anayeshikilia mali ya Benki hiyo ikiwa ni pamoja na kumbukumbu au nyaraka na vifaa vyovyyote vya ofisi anataarifiwa kwamba alipe madeni hayo, arudishe kumbukumbu/nyaraka na mali za benki hiyo kwa Mfilisi (DIB) kupitia anuani iliyotajwa hapo chini kabla ya siku ya Jumatatu tarehe 12 Juni, 2017. Wale watakaokaidi taarifa hii watachukuliwa kwamba wanashikilia mali hizo kinyume cha sheria kuanzia siku ya Jumatatu tarehe 12 Juni, 2017.
- (b) Vile vile, wadai wote ambao sio wenye amana (Depositors) wa **FBME Bank** (chini ya ufilisi) wanataarifiwa kuleta madai yao yakiwa na uthibitisho kamili kwa Mfilisi kwa kutumia anuani iliyotolewa hapo chini kabla ya siku ya Jumatatu tarehe 12 Juni, 2017.

Mkurugenzi

Bodi ya Bima ya Amana

Jengo la Makao Makuu ya Benki Kuu ya Tanzania

2 Mtaa wa Mirambo

Ghorofa ya 7, Mnara wa Kaskazini

11884 DAR ES SALAAM

Email: DIB-INFO@bot.go.tz

TEL: +255 22 223 5390

Fax: +255 22 223 4200

IMETOLEWA TAREHE 12 MEI, 2017